

Hii gazeti ina andikwa na shirika lisilokuwa la kiserekali Internews kwa ushirikiano na wizara ya afia na Shirikisho la Kimataifa la Msalaba Mwekunda na Jumuiya Nyekunda kwa kujibu kwenyi mahitaji za habari ya jamii.


Kila juma, tunakusanya na kuchambuwa maioni ya jamii (uvumi yani habari zenyi hazina uhakika, wasiwasi, maulizo, na kazalika) na tunatafuta majibu ku toka kwa wataalamu kwa kushirikisha jamii. Maulizo hizo zinachunguzwa kulingana na maana(umuhimu) yazo na mwendeleo wazo.

**YENYI TULISIKIA
JUU YA:**

SABABU GANI VYOMBO VYA KUNAWIA NDANI MIKONO HAVIONEKANE TENA MU FASI MINGI ZENYI ZINAWEZA KUFIKA AMO WATU WOTE PA BUTEMBO?

Fuateni habari za jibu juu ya Ebola katika gazeti ya Radio "Koma Ebola"

soundcloud.com/user-740750674
Facebook.com/komaebola
@Ebolakoma
koma-ebola.info



MAJIBU

Kutoonekana kwa vyombo vya kunawiamo mikono ma fasi ya watu wengi mujini Butembo inaweza tokana na sababu mbili:

1- Shirika la ukingo na uchunguzi wa maambukizi inayo husika na kugabula vyombo vya usafi kwa wanaokuwa na lazima navyo na kwa jamii yote, inafuutilia kazi ya kupana maji na kutengeneza vyombo. Wakati habipatikane, shirika hii inahakikisha kuwa binabadilishwa.

2- Inawezekana pia kuwa upotevu wa vitu iliotokea wakati ya upinzani ya kijamii Kwa sababu mara mingi wakati wa maandamano, vyombo vinaharibika ao vinaibiwa na watu wenyi nia mbaya. Njo kwa maana jamii inashauriwa kujitahidi kwa kulinda vyombo hivyo kwa kupiganisha vema zaidi magonjwa mbali mbali inayotokana na uchafu.


Ni ya lazma na ya muhimu kwa jamii kukuwa na mipango nzuri ya kukinga, kuuza ao kubadilisha vyombo kunako maeneo ili waendelee tabia nzuri za kunawa mikono.

**YENYI TULISIKIA
JUU YA:**

MIPANGO GANI INATAYARISHWA KWA UFUATILIAJI YA WALIO PONA KISHA HII UGONJWA YA EBOLA?

Fuateni habari za jibu juu ya Ebola katika gazeti ya Radio "Koma Ebola"

 soundcloud.com/user-740750674
 Facebook.com/komaebola
 @Ebolakoma
 koma-ebola.info



TULISIKIA PA BENI
March
(Mwezi ya Tatu)
2020

Chumba ya Waziri (Ministere) wa Afya ya Jamuhuri ya Kidemokwasia ya Congo haikungoya mwisho wa magonjwa kwa kuanza kufuatilia walio pona. Ilian芝sha mipango ya kufuatilia walio pona tangia mwezi wa kumi na moja 2018 (Novemba 2018), ikiwa miezi tatu pekee yake kisha mwanzo wa ugonjwa. Inapangilia kuendelesha ufuatiliaji hii mpaka kisha ata miaka mbili ao tatu kisha kutanganza mwisho wa ugonjwa kwa njia tatu zifuatazo:


- 1- Ufuatiliaji kimatumzo: Kitendo hii inahusika na kuchunguza kila siku hali ya afya ya walio pona kwa kuwashurulikia haraka (mbio) kama wanakuwa na shida za afya.
- 2- Ufuatiliaji wa kisaikolojia (hali ya akili): hii inaomba kusindikiza watu kwa njia ya shauri kwa kuwasaidia kurudia tena ndani ya jamii na kuzuia wasikuwe na mawazo mingi.
- 3- Ufuatiliaji ki bayolojia: Vipimo vitafanyika mara kwa mara kwa yule alie pona ili kujihakikishia maendeleo yake ya kiafya.
Inaombwa sana kwa walio pona Ebola na kwa jamii kuendelea kuheshimia hatua za ukingo.

**YENYI TULISIKIA
JUU YA:**

SABABU GANI WANAPANA CHANJO (NDUI) KWA KINGUVU SIKU HIZI?

Fuateni habari za jibu juu ya Ebola
katika gazeti ya Radio "Koma
Ebola"

 soundcloud.com/user-740750674
 Facebook.com/komaebola
 [@Ebolakoma](https://Twitter.com/@Ebolakoma)
 koma-ebola.info


MAJIBU

Chanjo (ndui) ya kuepuka Ebola haipaniwe kwa kinguvu. Inapanwa kisha kuitika bila mkazo kwa washiriki. Siku hizi, chanjo (ndui) inafanyika kwa njia ya kijiografia, ambayo ni kusema kufwatana na mahitaji katika eneo fulani ili kuongeza ukingo wa jamii zidi ya Ebola.

Inaombwa kwa jamii kujichanjisha kwa wakati ili wajikinge na Ebola.

Hii gazeti ina andikwa kwa msaada wa watu wa Amerika kupitia Shirika ya Amerika kwa maendeleo ya kimataifa (USAID). Yaliyomo haionyeshi maoni ya USAID na serikali ya Amerika.